Sasisho la COVID-19 katika Jiji la Burlington

Kituo cha Rasilimali na Kupona kwa COVID-19 cha Burlington (RRC)

Juni 2021

(Kiswahili) (Swahili)

Maangazio:

- Mipango ya Vijana kwa Majira ya Kiangazi
- Taarifa ya Chanjo ya COVID-19
- Mkakati wa Mafunzo ya Mapema – Utunzaji wa Mtoto wa Bei Nafuu
- Matukio ya Bila Malipo katika Majira ya Kiangazi kwa Familia
- Milo ya Bila Malipo katika Majira ya Kiangazi kwa Vijana Walio na Umri wa Miaka 18 na Chini
- VERAP – Mpango wa Usaidizi wa Dharura ya Kodi ya Nyumba katika Vermont
- Kuendelea, Kupiga Hatua - Mpango wa mafunzo ya Kazi ya Msaidizi wa Muuguzi Aliye na Leseni (LNA)
- Uchunguzi Mkuu wa Polisi katika Burlington

Mipango ya Vijana kwa Majira ya Kiangazi

Mnamo Juni tarehe 2, Meya Miro Weinberger alitangaza lengo la mipango ya vijana na shughuli za familia kwa majira ya kiangazi 2021. **Asante kwa uwekezaji wa zaidi ya $400,000 kutoka kwa Mpango wa kitaifa wa Uopozi Marekani, Jiji la Burlington limepokea fedha za kuboresha ufikiaji wa mipango ya majira ya kiangazi ya bila malipo au bei iliyopunguzwa na kupanua nafasi za mipango ya vijana.**

Mipango iliyopanuliwa na ushirikiano unajumuisha ofa kutoka kwa:

- Sanaa ya Jiji la Burlington - https://www.burlingtoncityarts.org/adult-youth-and-family-classes
- Mbuga za Burlington, Maeneo ya Kutulia na ya Maji Yanayotiririka - https://enjoyburlington.com/youth-camps/
- Fletcher Free Library - https://www.fletcherfree.org/
- Kituo cha King Street
- Sara Holbrook
- Kituo cha Flynn
- Wilaya ya Shule ya Burlington

Kati ya mipango ya kushiriki, kutakuwa na chaguo mbalimbali ikijumuisha kambi za siku nusu au siku nzima, na chaguo zote mbili za wiki fupi na anuwai. Huku kambi tofauti zitakuwa na malengo tofauti, watoto wanaweza kutarajia chaguo za shughuli kama vile uvumbuzi, spoti, sanaa na ufundi, kusoma, elimu, na zaidi nje ya nyumba!

Kwa maswali kuhusu kinachopatikana kwa sasa na jinsi ya kutuma ombi, tafadhali wasiliana na RRC kupitia recovery@burlingtonvt.gov au 802-755-7239. Usaidizi wa mkalimani wa simu unapatikana.

Chanjo za COVID-19

Kila mara huwa ni wazo zuri la kujilinda wewe na familia yako dhidi ya COVID-19! Ikiwa unahitaji usaidizi wa kujisajili bila malipo na chanjo salama kwa mtu yeyote aliye na umri wa miaka 12 na zaidi tafadhali pigia RRC simu kupitia 802-755-7239, AALV kupitia 802-985-3106, au USCRI kupitia 802-655-1963 ili kuunganishwa na kliniki.

Mkakati wa Mafunzo ya Mapema – Utunzaji wa Mtoto wa Bei Nafuu

Mipango ya
Ufadhili wa Elimu

Je, unahitaji usaidizi wa kulipia utunzaji wa mtoto? Mtoto wako anaweza kufuzu kwa Mpango wa Ufadhili wa Masomo wa Hatua za Kwanza

Familia zinazostahiki zinaweza kupokea ***Ufadhili wa Masomo wa Hatua za Kwanza*** kupitia Jiji la Burlington, ili kusaidia kwa gharama za masomo kwa utunzaji mtoto wa muda wote katika mipango iliyofuzu! Kuomba, familia zinahitaji kuwa wakazi wa Burlington, wanatimiza miongozo fulani ya mapato, na wana mtoto aliye na umri wa wiki 8 hadi miaka 2 ½.

JINSI YA KUTUMA OMBI:
Maombi yanakubaliwa kwa kipindi cha kutuma maombi ya ufadhili wa masomo cha 2020–2021. Kutuma ombi, piga simu au tuma barua pepe kwa Paula Bonnie kupitia paula@letsgrowkids.org au 802-398-5464. Pia unaweza kuwasiliana na Kituo cha Simu cha RRC kupitia 802-755-7239 ili kupata usaidizi. Mkalimani kupitia kwa simu ya mkononi zinapatikana.

Jifunze zaidi katika www.burlingtonvt.gov/it/earlylearning.

Matukio ya BILA MALIPO katika Majira ya Kiangazi kwa Familia

DENSI YA KURUKARUKA – Kila Ijumaa kuanzia Juni 4 – Septemba 10
Watoto watakuwa na burudani msimu huu wa kiangazi katika maji ya kurukaruka ya Mbuga ya Jumba Kuu la Jiji (City Hall Park)! Chemichemi ya maji yenye mwangaza kadhaa, inaweza kufikiwa kwa kiti cha magurudumu itakuwa moja kwa moja msimu huu wa joto kwa Densi ya Kurukaruka. Kwa Ijumaa 15, DJ wa ndani watacheza midundo inayofaa familia huku chemichemi ya maji ikiendelea kutoa maji. Familia zitaanzisha kila wikendi kwa kucheza zamu ya kubadilika ya DJ bora kwatika mpango huu wa kwanza kabisa.

MISURURU YA TAMASHA YA KISIKUSIKU – kila Ijumaa na Jumamosi saa 1 jioni, kuanzia Juni tarehe 18
Hii ni misururu mipya ya tamasha inayowasilisha bendi bora za Vermont katika mazingira ya jioni ya mapenzi katikati ya mji.

JUMAMOSI ZA SANAA YA FAMILIA – Kila Jumamosi ya 4 ya mwezi (tukio lijalo ni Juni tarehe 26 saa 5 asubuhi hadi saa 7 mchana)
Familia zimealikwa kufika kwenye varanda ya Kituo cha Sanaa cha Jiji la Burlington ili kuunda sanaa zao wenyewe huku wakihimizwa na maonyesho ya sanaa ya sasa. Kila Jumamosi ya Sanaa ya Familia ni ya bila malipo na hutoa mradi tofauti wa uundaji sanaa ambao utachochea fikira za wanafamilia yako.

Milo ya Bila Malipo katika Majira ya Kiangazi kwa Vijana Walio na Umri wa Miaka 18 na Chini

Mahitaji ya lishe ya wanafunzi huwa hayasimami shule zikifungwa. Saidia wanafunzi kufurahia msimu wa kiangazi kwa chakula mbichi na vya ndani! Mradi wa Chakula Shuleni katika Burlington hutoa vyakula vya bila malipo kwa watoto na wanarika wote msimu wa kiangazi. Hakuna ombi au usajili unaohitajika! Fika tu muda wa chakula ulioorodheshwa hapa chini.

Saa za Msimu wa Kiangazi wa 2021 - Juni 21 hadi Agosti 20
Inapatikana Jumatatu hadi Ijumaa



Maghorofa ya Riverside Apartments
Chakula cha mchana saa 5:00 asubuhi hadi saa 8:00 mchana (Inapakuliwa saa 6 mchana)
Maghorofa ya South Meadow Apartments
Chakula cha mchana saa 5:00 asubuhi hadi saa 8:00 mchana (Inapakuliwa saa 6 mchana)
Maghorofa ya Franklin Square Apartments
Chakula cha mchana saa 5:00 asubuhi hadi saa 8:00 mchana (Inapakuliwa saa 6 mchana)
Kumbwe saa 11:00 jioni hadi saa 1:00 jioni (Inapakuliwa saa 11:30 jioni)
Roosevelt Park
57 Oak Street, Burlington
Chakula cha jioni 10:00 jioni hadi saa 12:30 jioni (Inapakuliwa saa 11 jioni)
Mpya! City Hall Park
Nyuma ya City Hall, Barabara ya 149 Church Street
Chakula cha mchana saa 5:00 asubuhi hadi saa 8:00 mchana (Inapakuliwa saa 6 mchana)
Mpya! CP Smith Elementary School
332 Ethan Allen Pkwy
Kumbwe 7:00 mchana hadi saa 10:00 jioni (Inapakuliwa saa 2 mchana)

Ili kupata taarifa kuhusu vyakula vya bila malipo vya msimu wa kiangazi vilivyo karibu nawe mahali popote katika Vermont, piga 2-1-1 (huduma za mkalimani kwa simu zinapatikana) or tuma neno FOOD kwa 877-877 (Kiingereza).

Mpango wa Usaidizi wa Dharura ya Kodi ya Nyumba katika Vermont

JE, UNAHITAJI USAIDIZI WA KULIPA KODI YA NYUMBA?

Usaidizi wa kodi ya nyumba na bili ya matumizi unapatikana ili kuwasaidia watu wa Vermont kuepuka kuondolewa kwa nyumba na kulipa bili zao za matumizi!

Mpango huo husaidia kaya kwa kulipa **salio za kodi za sasa na zilizopita, matumizi na gharama za kawi ya nyumbani ya sasa na zilizopita, na matumizi mengine yanayohusiana na nyumba**. Usaidizi wa matumizi unaweza kujumuisha umeme, gesi, maji, taka, kuondolewa kwa takataka na gharama za kawi, kama vile mafuta. Maombi yatahitaji kukamislishwa na mkodishaji na mmiliki wa mali hiyo, na malipo ya moja kwa moja yatafanywa kwa mmiliki.

Tovuti: https://erap.vsha.org/ (Tafsiri zinapatikana)

Kwa ajili ya Usaidizi wa Maombi na Msaada wa Lugha, wasiliana na:

AALV - Muungano wa Waafrika Wanaoishi katika Vermont
http://www.aalv-vt.org/
(802) 985-3106

CVOEO - Mradi wa Uwezeshaji wa Kifedha kwa Wamarekani Wapya
https://www.cvoeo.org/
(802) 860-1417 x117

USCRI Vermont - Kamati ya Marekani ya Wakimbizi na Wahamiaji
https://refugees.org/uscri-vermont/
(802) 655-1963

Kuendelea, Kupiga Hatua

UKO TAYARI KWA MABADILIKO?
Anza KAZI MPYA katika huduma ya afya na KUPIGA HATUA!

Pata MAPATO YA JUU kama Msaidizi wa Muuguzi Aliye na Leseni (LNA). Mpango huu wa wiki 10 ni wa BILA MALIPO kwa waombaji wanaostahiki, ambao pia watalipwa kwa ajili ya mafunzo yao. Misaada ya zaida ya masomo itatolewa. Kozi hii itatolewa mtandaoni na darasani ana kwa ana, usiku tatu kwa wiki.

Vipindi Vijavyo vya Mafunzo Yataanza:

- Julai 13
- Septemba tarehe 8
- Oktoba tarehe 26
- Desemba tarehe 13

Kutuma Ombi:
Tembelea www.burlingtonvt.gov/covid-19/LNA
Kwa maswali, tuma barua pepe kwa gnanton@burlingtonvt.gov.

Uchunguzi Mkuu wa Polisi katika Burlington

Jiji la Burlington kwa sasa linatafuta polisi mkuu anayefuata! Jiji lina matumaini ya kukusanya maoni kutoka kwa jumuiya kuhusu sifa ambazo wangependa kuona katika kiongozi anayefuata wa idara ya polisi, sawa na kipaumbele ambacho idara ya polisi inafaa kuwa nacho baadaye. Uchunguzi huu umetafsiriwa katika lugha 8 tofauti, na unaweza kubadilishwa kwa lugha tofauti kwa kutumia kitufe katika sehemu ya juu upande wa kulia.

Fanya uchunguzi huo: https://www.surveymonkey.com/r/btv_police_chief_search

Maswali? Je, Unahitaji Usaidizi?

Kituo cha Rasilimali na Kupona kwa COVID-19 (RRC) cha Burlington kiko hapa kukusaidia, wasiliana nasi kupitia 802-755-7239 au recovery@burlingtonvt.gov na uache ujumbe wenye jina lako, lugha unayopendelea, na maelezo ya mawasiliano na tutakusaidia haraka iwezekanavyo. Kituo chetu cha kupokea simu kina huduma za ukalimani kwa simu. Saa zetu za kufanya kazi ni Jumatatu hadi Ijumaa, 2:00 asubuhi hadi 10:30 jioni.

Pata Tafsiri:

Idara ya Afya ya Vermont
https://www.healthvermont.gov/media/translation/covid-19-translations
Jiji la Burlington
https://www.burlingtonvt.gov/covid-19/translated
Jopo Kazi la Lugha Anuwai katika Vermont:
https://www.youtube.com/channel/UC3zjPpeFnXqvESr1y3d4DvQ

Taarifa katika waraka huu inaweza kubadilika jinsi miongozo inasasishwa katika kiwango cha kitaifa na jimbo.